



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUAHIRISHA UCHAGUZI KATIKA KATA YA
KAGERA NKANDA ILIYOPO KASULU DC**

Dar es Salaam, 13 Septemba, 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa umma juu ya kuahirisha shughuli za uchaguzi katika kata ya Kagera Nkanda. Hatua hiyo inatokana na uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma tarehe 20 Agosti, 2021 juu ya maombi ya Diwani wa Kata hiyo ya Kagera Nkanda.

Tume katika kikao chake cha tarehe 13 Septemba, 2021, imezingatia uamuzi huo na kwa mamlaka iliyonayo chini ya kifungu cha 41(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura 292, imeamua kuahirisha shughuli za uchaguzi katika Kata ya Kagera Nkanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Aidha, shughuli za uchaguzi mdogo katika majimbo mawili ya Konde, Pemba na Ushetu, Shinyanga pamoja na kata 9 zilizopo katika halmashauri mbalimbali za Tanzania Bara zitaendelea kama zilivyopangwa awali na Tume.


Dkt. Wilson Mahera Charles
MKURUGENZI WA UCHAGUZI